



TAARIFA KWA UMMA

24 Septemba, 2018

UPOTOSHAJI KUHUSU UWEPO WA VIDONGE VYENYE DAWA YENYE MADHARA KWENYE CHUPA ZA CHAI (THERMOS)

1. Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi za Serikali zilizo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zenye wajibu wa kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa.
2. Hivi karibuni kumekuwepo na video inayosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu vidonge vilivyopo kwenye baadhi ya chupa za chai kuwa ni vidonge vyenye dawa yenye madhara kwa watumiaji na video nyingine ya lugha ya kiarabu ikieleza kuwa vidonge hivyo vina madini ya *asbestos*.
3. TBS na TFDA wanapenda kuwatoa hofu wananchi kuwa vilivyomo ndani ya chupa za chai vyenye umbo kama la vidonge sio dawa na wala sio sumu bali ni vitu vilivyotengenezwa kwa kutumia karatasi ambayo ni teknolojia ya kisasa inayotumika kutenganisha kuta mbili za chupa ili kutunza joto la kimiminika kilichowekwa kwenye chupa husika.
4. Taasisi zote mbili zinawahakikishia wananchi kuwa bidhaa hizo ni salama kwa matumizi ya kutunza joto la kimiminika kama vile chai.
5. Rai inatolewa kwa wananchi kuepuka kusambaza taarifa kupitia mitandao ya kijamii zisizohakikiwa na TBS na TFDA ili kuondoa hofu na taharuki zisizo za lazima. Wananchi wanaombwa kutoa taarifa katika ofisi za makao makuu au kanda za TBS au TFDA zilizopo katibu au ofisi za waganga wakuu wa Wilaya au Mikoa pindi wanapokuwa na mashaka juu ya usalama na ubora wa bidhaa ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wakati.

Imetolewa na;

**Mkurugenzi Mkuu,
Shirika la Viwango Tanzania,
S.L.P 9524, Dar es Salaam.**

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa,
S.L.P 77150, Dar es Salaam.**

**Simu: +255 22 2450206/2450949/2450298/
Hotline: 0800110827
Nukushi: +255 22 2450959
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: www.tbs.go.tz**

**Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751/
658 445222/777 700 002/685 701735
Hotline: 0800110084
Nukushi: +255 22 2450793
Barua pepe: info@tfda.go.tz
Tovuti: www.tfda.go.tz**

